HOTUBA YA MHE. ANNA E. MGHWIRA,
MKUU WA MKOA WA KILIMANJARO WAKATI
WA MAPOKEZI YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU
KUTOKA MKOA WA MANYARA TAREHE 15/09/2017

- Mheshimiwa Joel N. Bendera - Mkuu wa Mkoa wa Manyara;
- Ndugu Viongozi wa Serikali na Vyama vya Siasa wa Mikoa ya Kilimanjaro na Manyara;
- Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa;
- Ndugu Wakimbiza Mwenge Kitaifa kwa mwaka 2017;
- Ndugu Wajumbe wa Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa ya Kilimanjaro na Manyara;
- Ndugu Wakuu wa Wilaya za Mkoa wa Kilimanjaro na Manyara;
- Ndugu Wenyeviti na Mameya wa Halmashauri za Wilaya na Manispaa;
- Waandishi wa Habari;
- Mabibi na Mabwana:

Ndugu Mkuu wa Mkoa wa Manyara;

Kwa niaba ya viongozi na wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro ninamshukuru Mungu aliyetuwezesha kukutana katika eneo hili la Kijiji cha Ormelili lililoandaliwa maalum kwa ajili ya makabidhiano ya Mwenge wa Uhuru kwa mwaka huu wa 2017 kati ya Mkoa wa Manyara na Kilimanjaro huku tukiwa wenye nguvu na afya njema.

Ninapenda pia kutumia nafasi hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa viongozi na wananchi wote wa Mkoa wa Manyara kwa kazi nzuri mliyoifanya ya kumaliza salama mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2017. **Hongereni Sana!**

Aidha, ninawapongeza Wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa wakiongozwa na **Ndugu Amour Hamad Amour** kwa kazi nzuri waliyoifanya katika Mkoa wa Manyara; Kwa upendo, Uzalendo na moyo mkunjufu ninawakaribisha sana Mkoani Kilimanjaro kwenye chimbuko la Mwenge wa Uhuru, kwani kila mtanzania anajua kuwa Mwenge wa Uhuru ulipowashwa kwa mara ya kwanza ulipandishwa juu ya kilele cha mlima Kilimanjaro; hivyo basi leo Mwenge wa Uhuru umekuja nyumbani.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru;

Mkoa wa Kilimanjaro una historia nzuri ya kuuenzi Mwenge wa Uhuru na kutekeleza kwa vitendo maudhui yote yanayoainishwa kwenye ujumbe wa Mwenge wa Uhuru kila mwaka. Mwaka huu ujumbe wa Mwenge wa Uhuru unasema, *nanukuu* **"Shiriki Kukuza Uchumi wa Viwanda kwa Maendele ya nchi yetu".** *Mwisho wa kunukuu.*

Ujumbe wa Mwenge una umuhimu maalum kwa Mkoa wetu. Mkoa huu umebahatika kupata uzoefu wa kutumia uchumi wa viwanda. Tangu Uhuru, Serikali imeelekeza ujenzi wa viwanda mbalimbali katika Mkoa wetu ambavyo viliweza kutoa ajira nyingi kwa sehemu kubwa ya jamii yetu.

Uzoefu wa uchumi wa viwanda unafahamika na kuheshimika kwa mchango wake kwa maendeleo ya mtu mmoja mmoja na jamii nzima ya Mkoa huu.

Aidha, baadhi ya wakazi wa Kilimanjaro wameanzisha viwanda binafsi katika nyanja mbalimbali zinazotoa ajira kwa wananchi.

- Kwa sababu hii, viongozi na wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro tunajivunia utaratibu uliowekwa na Serikali

katika kurejesha viwanda ambavyo vilibinafsishwa na havifanyi kazi.

- Kwa mwitikio wa msukumo huu, Serikali ya Mkoa wa Kilimanjaro imetoa kipaumbele katika kuhakikisha maelekezo haya ya Serikali yanafanikiwa ili viwanda vipatavyo sita **(6)** viweze kufanya kazi na kuweza kuongeza uchumi wa Mkoa.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru;

Mkoa wa Kilimanjaro kama ilivyo Mikoa mingine, umeathiriwa na janga la ugonjwa wa UKIMWI. Hata hivyo, unaendelea na juhudi za kuwahimiza wananchi na kuwakumbusha umuhimu wa kushiriki katika mapambano dhidi ya ugonjwa huu hususan katika kubadili tabia hatarishi ambazo zinawaweka katika hatari ya kupata maambukizi ya virusi vya UKIMWI.

Aidha juhudi za kutoa elimu kwa walioathirika na virusi ya UKIMWI zinaendelea kutolewa ili kufikia lengo la kuhakikisha hawapati maambukizi mapya na afya zao zinaendelee kuimarika.

Kwa mujibu wa takwimu za Mkoa za viashiria vya VVU, kiwango cha maambukizi ya VVU kimepungua kutoka asilimia **7.3** (kwa mujibu wa utafiti wa viashiria vya VVU mwaka **2003/2004**) na

kufikia asilimia **3.4** (kwa mujibu wa utafiti wa viashiria vya VVU mwaka **2011/2012**)**.**

Mkoa wa Kilimanjaro ni kati ya Mikoa iliyo na kiwango kidogo cha maambukizi ukilinganisha na takwimu za Kitaifa ambapo Tanzania ni asilimia **5.1.**

Aidha, kuhusu maambukizi ya VVU miongoni mwa akinamama wajawazito, kiwango cha maambukizi kimeshuka kutoka asilimia **3.3** mwaka **2009** hadi asilimia **1.8** mwaka **2016.**

Kimsingi mafanikio hayo yanatokana na juhudi za wadau mbalimbali kwa kushirikiana na Serikali. Aidha, bado juhudi za pamoja zinahitajika ili kupunguza ongezeko la maambukizi ya VVU hususan kwa kundi la vijana.

Mkoa umejipanga ili kuhakikisha kuwa, maambukizi yanapungua kwa kuelimisha wananchi kuacha tabia hatarishi na vitendo vinavyoongeza maambukizi. Aidha, Mkoa unahamasisha upimaji wa hiari na matumizi ya dawa kwa watu ambao wamegundulika kuwa wanaishi na maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Aidha, Mkoa unatekeleza mkakati wa Kimataifa wa kufikia malengo ya 90 tatu ifikapo mwaka 2020 yaani asilimia 90 ya walioambukizwa VVU wawe wamepimwa na kugundulika, 90 ya pili ni asilimia 90

ya wale waliogundulika kuwa na VVU wameazishiwa dawa za kufubaza VVU (ARVs) na 90 ya tatu ni asilimia 90 ya waliooanzishiwa ARVs wawe na virusi vilivyofubazwa kwa kiwango kilichowekwa.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru;

Mbio za Mwenge wa Uhuru zinatukumbusha pia kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa. Serikali ya Mkoa inaendelea kupambana na kukabiliana na tatizo la watoa na wapokea rushwa ikizingatiwa jinsi wanavyobadili mbinu za kufanya vitendo hivyo.

Kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Serikali ya Mkoa imelazimika kujifunza mbinu mbalimbali za kukabiliana na tatizo hili. Kupitia ushirikiano huu katika kipindi cha kuanzia **Juni, 2016** hadi Juni, **2017,** taarifa za rushwa zipatazo **247** zimepokelewa kupitia vyanzo mbalimbali vya kiuchunguzi. Katika taarifa hizo, taarifa **247** zimeonekana kuwa na uhusiano na rushwa, na kati ya taarifa hizo taarifa **21** zipo katika hatua mbalimbali kwa ajili ya kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Jumla ya kesi **29** zimefikishwa Mahakamani na kesi **4** zimehukumiwa. Kesi za rushwa zinazoendelea Mahakamani ni **25.** Aidha, taarifa **168** zipo katika hatua za awali za uchunguzi.

Aidha kwa mwaka 2016/2017 kiasi cha fedha za Serikali zilizookolewa kupitia vita dhidi ya rushwa ni shilingi **86,350,313/=.**

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru;

Kijiografia Mkoa wa Kilimanjaro, unapakana na nchi jirani ya Kenya, kwa hiyo kuna muingiliano katika shughuli mbalimbali za kimaisha hasa kutokana na kuimarika kwa miundombinu iliyoboreshwa kama barabara na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA).

Aidha, uwepo wa fursa hizi imekuwa changamoto katika Mkoa wetu kwani raia wasio waaminifu wanatumia fursa hizi kuingiza, kusafirisha na kusambaza dawa za kulevya.

Serikali ya Mkoa kupitia Jeshi la Polisi imekuwa mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya uingizaji, usafirishaji, usambazaji na matumizi ya dawa za kulevya.

Katika kipindi cha kuanzia mwezi **Julai, 2016** hadi **Julai, 2017**, Jeshi la Polisi limefanikiwa kukamata aina mbalimbali za dawa za

kulevya kama ifuatavyo: Bhangi kg. **966,** Mirungi kg**. 5,502.7** na Heroine gm. **16.15.** Katika matukio hayo watuhumiwa **799 (Me 699 na Ke 100)** walikamatwa, kesi **550** zimefikishwa Mahakamani na kesi **131** zimeisha na zinazoendelea kusikilizwa ni kesi **419.**

Aidha, Serikali ya Mkoa inaendelea kuhamasisha jamii kudhibiti na kutokomeza dawa za kulevya ikiwa ni njia ya kunusuru vijana ambao wanapata madhara ya kiafya yakiwemo magonjwa ya akili, mapafu, moyo, ini, figo, mtindio wa ubongo na hatimaye kusababisha vifo vya ghafla. Madhara haya yanasababisha kukosa vijana wa kusukuma mbele maendeleo ya Taifa letu.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru;

Mkoa wa Kilimanjaro pia umeathiriwa na ugonjwa wa malaria. Mkoa unaendelea na juhudi za kuwahamasisha wananchi kupambana na ugonjwa huu.

Kwa mujibu wa Takwimu, hadi kufikia mwaka **2016,** takwimu zinaonyesha kuwa hali ya maambukizi ya malaria kwa Mkoa ni asilimia **1.** Mgawanyiko wa maambukizi Kiwilaya ni kama ifuatavyo:-

- Wilaya ya Hai inaonyesha kuwa na maambukizi kidogo ya **0.2%**. Aidha takwimu zinaonyesha kuwa, watoto chini ya

miaka mitano **(5)** na akina Mama Wajawazito hasa waliopo Vijijini ndio wanaoathirika zaidi.

Mkoa umejipanga kuhakikisha kuwa, tunapunguza vifo vya watoto na wakina Mama vitokanavyo na Malaria kwa kutoa elimu ya afya na kuhakikisha dawa za malaria zinapatikana katika Vituo vya Huduma za Afya, kuhimiza wananchi hasa kina-Mama wajawazito kutumia vyandarua; kwa mwaka huu jumla ya vyandarua **989,091** vimetolewa kwa wananchi. Aidha, wananchi wanahimizwa kufanya usafi wa mazingira kuzunguka makazi yao ili kuzuia mazalia ya mbu na kutumia vituo vya huduma vilivyopo karibu nao pindi wanapohisi dalili za malaria.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru;

Mwenge wa Uhuru ukiwa Mkoani Kilimanjaro utapata fursa ya kutembelea jumla ya miradi **42** ya maendeleo katika Halmashauri **7** za Mkoa wetu. Katika miradi hiyo, miradi **18** ni ya kufunguliwa/kuzinduliwa, miradi **14** ni ya kuwekewa mawe ya msingi na miradi **10** ni ya kutembelewa na baadhi ya miradi hiyo wahusika watapatiwa mikopo. Fedha zilizotumika na zinazoendelea kutumika katika kukamilisha miradi hiyo ni shilingi **12,387,533,173/=** (shilingi bilioni kumi na mbili, milioni mia

tatu na themanini na saba, laki tano na thelathini na tatu elfu na mia moja na sabini na tatu tu).

Miradi ya Mwenge wa Uhuru kwa 2017 imechangiwa na Serikali na wadau wengine wa maendeleo katika mchanganuo ufuatao:-

1. Serikali Kuu imechangia shilingi **5,228,484,717/=** (shilingi bilioni tano, milioni mia mbili ishirini na nane , laki nne themanini na nne elfu, mia saba kumi na saba tu);

2. Halmashauri za Wilaya na Manispaa zimechangia shilingi **1,025,594,000/=** (shilingi bilioni moja na milioni ishirini na tano, laki tano na tisini na nne elfu tu);

3. Michango ya fedha na nguvu za wananchi ni shilingi **3,055,975,257/=** (shilingi bilioni tatu na milioni hamsini na tano, laki tisa sabini na tano elfu, mia mbili hamsini na saba tu);

4. Wahisani (Wafadhali mbalimbali) ni shilingi **3,077,479,198/=** (shilingi bilioni tatu na milioni sabini na saba, laki nne sabini na tisa elfu, moja elfu, mia moja tisini na nane);

Miradi yote hii imegusa sekta zote muhimu ambazo ni: elimu miradi **10,** Afya miradi **4,** maji miradi **4,** kilimo, ufugaji na uvuvi miradi **5, m**iradi ya viwanda **9**, barabara miradi **4** na miradi mingineyo **6.**

Ni mategemeo yetu kuwa Mwenge wa Uhuru utakapokuwa Mkoani Kilimanjaro utaimarisha na kuibua ari mpya, umoja na mshikamano wa wana-Kilimanjaro katika kuchangia miradi ya maendeleo.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru;

Kutokana na ratiba tuliyoiandaa, tarehe **15/09/2017**, Mkoa wa Kilimanjaro tunapokea Mwenge wa Uhuru kutoka Mkoa wa Manyara na utakimbizwa katika Wilaya ya Siha leo. Aidha:-

- Tarehe 16/09/2017 – Utakuwa Wilaya ya Hai
- Tarehe 17/09/2017 – Utakuwa Manispaa ya Moshi
- Tarehe 18/09/2017 – Utakuwa Halmashauri ya Moshi
- Tarehe 19/09/2017 – Utakuwa Wilaya ya Rombo
- Tarehe 20/09/2017 – Utakuwa Wilaya ya Mwanga
- Tarehe 21/09/2017 – Utakuwa Wilaya ya Same
- Tarehe 22/09/2017 – Tutakabidhi Mwenge kwa wenzetu wa Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara;

Naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe binafsi, viongozi na wananchi wa Mkoa wa Manyara kwa kutukabidhi Mwenge wa Uhuru ukiwa salama pamoja na vijana sita (6) wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa wakiwa salama na wenye afya njema na nguvu, na mimi kwa niaba ya viongozi na wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro ninaahidi kuwatunza vyema na kuhakikisha wanapata huduma nzuri kwa kadri itakavyowezekana ili vijana hawa waweze kutekeleza jukumu hili la Kitaifa hadi tutakapowakabidhi wenzetu wa Mkoa wa Tanga ifikapo tarehe **22/09/2017**.

Ndugu Vijana Wakimbiza Mwenge Kitaifa;

Kwa niaba ya viongozi na wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro; ninaomba kutumia fursa hii **kuwakaribisha sana Mkoani Kilimanjaro.**

Ninawatakia mbio njema, afya njema na ninawaahidi **ushirikiano wa dhati kutoka kwangu, mimi binafsi, viongozi wenzangu** na **wananchi wote wa Mkoa wa Kilimanjaro.**

AHSANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA.

MWENGE HOYEEEE!!!!!!